


# Mwongozo wa haraka kuhusu chanjo ya virusi vya korona

Maelezo mafupi kutoka kwa Taasisi ya Afya ya Umma ya Norwe (Norwegian Institute of Public Health) kuhusu chanjo ya kuzuia kuambukizwa COVID-19 (virusi vya korona).

---




## Ni nani atakayepokea chanjo ya virusi vya korona?

Kila mtu anayependekezwa kupokea chanjo.

Chanjo hailipishwi.

---




## Je, unapokea chanjo kwa njia gani?

Chanjo inatolewa kama sindano inayodungwa kwenye mkono.

Chanjo inatolewa kama vipimo viwili vya dawa kwa tofauti ya wiki chache.

Kumbuka kusema ikiwa una mizio, unatumia dawa au iwapo wewe ni mgonjwa.

---



## Je, chanjo inasaidia kwa njia gani?

Chanjo inakuzuia kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19.

Watu wengi hulindwa dhidi ya maambukizi baada ya wiki 1 hadi 2 baada ya kupokea chanjo ya pili.

Watu ambao wamechanjwa bado wanapaswa kufuata ushauri wa kukomesha kusambazwa kwa virusi vya korona.




## Je, chanjo inafanya kazi vipi?

Chanjo huufunza mwili kutambua na kujilinda dhidi ya kuambukizwa virusi vya korona.

Chanjo huondolewa mwili kwa haraka.

Hata hivyo, mwili hukumbuka jinsi ya kujilinda dhidi ya kuambukizwa virusi hivyo.




## Madhara ya chanjo

Chanjo imejaribiwa kwa kufanywa kwa tafiti kubwa kwa maelfu ya watu. Madhara ya kawaida ya chanjo ni:

- kuhisi uchungu mahali ulipodungwa sindano
- uchovu
- kuumwa na kichwa
- maumivu ya mwili
- kuongezeka kwa joto mwili au kuhisi baridi

Madhara haya yanakufanya usijihisi vizuri, lakini hutoweka baada siku chache.



## Madhara ya chanjo yasiyo ya kawaida

Wasiliana na daktari au mtaalamu mwingine wa afya ikiwa una dalili ambazo hazitarajiwi, kali au ambazo zinadumu kwa muda mrefu baada ya kupokea chanjo.